**SHINYANGA REGION COOPERATIVE UNION**
**P. O. BOX 349, SHINYANGA, TEL/FAX 255 28 2762525**
Email:info@shireculimited.co.tz Website:www.shireculimited.co.tz

**KUMB. NA.SRCU/TB/39/VOL.II/106** **TAREHE:** 6/01/2026

**TANGAZO LA KAZI ZA UFUNDI WA MAJENGO – FUNDI JAMII ( LOCAL FUNDI )**

1. Chama kikuu cha Ushirika Mkoa wa Shinyanga ni Chama kilichosajiliwa kwa **Na.AFF-SHY-SHY-MC-2022-9** na hufanya kazi chini ya sheria ya Vyama vya Ushirika Namba **6** ya mwaka **2013** pamoja na kanuni zake za mwaka **2015.** Maeneo ya shughuli za Chama hiki ni Mkoa wa Shinyanga katika Wilaya ya Shinyanga Mjini, Shinyanga Vijijini na Kishapu.
2. Chama kikuu cha Ushirika SHIRECU (1984) LTD kwa mwaka wa fedha wa 2025/2026 kinatarajia kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo ikiwa ni pamoja na ukarabati wa shule ya Sekondari ya Buluba iliyopo Shinyanga Mjini

3. Kwa idhini ya Bodi ya chama Kikuu, Mwenyekiti wa bodi anatangaza Kazi za ufundi wa majengo kwa njia ya Kotesheni shindanishi kwa kazi za kupaka rangi majengo, kazi ya uselemala, kazi uashi, kazi ya ufundi bomba, Kazi ya kukarabati madirisha ya vioo.

**A. MAHITAJI YA KOTESHENI.**

| AINA YA KAZI | NAMBA YA KOTESHENI |
|---|---|
| KUPAKA RANGI MAJENGO | SRCU/2025-2026/KTN/KPR/MJG/ 01 |
| KAZI YA USELEMALA | SRCU/2025-2026/KTN/KZY/USL/ 02 |
| KAZI YA UASHI | SRCU/2025-2026/KTN/KZY/USH/ 03 |
| KAZI YA KURABATI MADIRISHA YA VIOO | SRCU/2025-2026/KTN/KZY/KMV/ 04 |

4. Fundi mmoja anaruhusiwa kuomba kazi zaidi ya moja endapo atakuwa amethibitisha kuwa na uwezo.

5. Mchakato wa zabuni hii utafanyika kwa njia shindanishi ya Hati msako ( Kotesheni shindanishi ) kwa mujibu wa Mwongozo wa Ununuzi na Ugavi wa vyama vya Ushirika Tanzania Bara na Sheria na Kanuni za ununuzi wa umma na Kotesheni ya wazi kwa mafundi wote wenye sifa zinazohitajika.

6. Kila muombaji anatakiwa kujaza vitabu vya maelekezo na gharama (Schedule of labour) ambavyo vinapatikana kwenye ofisi ya Makao makuu ya SHIRECU(1984)LTD Kitengo cha manunuzi.

7. Waombaji wawasilishe Kotesheni zao zikiwa zimefungwa kwenye bahasha kwa umakini na kutiwa **lakiri.**

8. Mwombaji akishajaza kitabu atakiweka katika bahasha akiambatanisha na barua ya maombi ya kazi atakayoiomba na nyaraka muhimu za kiufundi kisha juu ya bahasha

ataandika **JINA LA AINA YA KAZI ANAYOIOMBA** na **NAMBA YA KOTESHENI** na siyo jina la muombaji. **ZINGATIA KUTOANDIKA JINA LAKO JUU YA BAHASHA**

9. Muda wa kutuma maombi ya Koteshenì ni siku saba 7 baada ya Tangazo kutolewa kuanzia tarehe 06 January, 2026 hadi tarehe 12 January 2026 saa Nne kamili asubuhi na SIKU HIYO NDIO SIKU YA MWISHO KUPOKEA KOTESHENI.

10. Koteshi zitakazochelewa hazitapokelewa wala hazitafanyiwa kazi wakati wa tathimini ya kotesheni hizo bila kujali sababu zozote za kuchelewa kwazo.

**B. SIFA ZA JUMLA ZA MWOMBAJI**

i. Awe na cheti cha ufundi kutoka chuo cha ufundi kinachotambulika na serikali
ii. Awetayari kuheshimu mkataba wa kazi atakayopewa.
iii. Awe anajua kusoma michoro na ramani za Majengo.
iv. Awe na uwezo wa nguvu kazi ya kutosha na uzoefu wa kujenga majengo mbalimbali
v. Awe na Vitendea kazi vya kutosha.
vi. Awe na Akaunti ya benki kwa ajilii ya malipo yake ya kazi atakazokuwa anazifanya.
vii. Waombaji wote ni lazima wawe ni raia wa Tanzania
viii. Waombaji wawe na kitambulisho cha NIDA.

**MAOMBI YOTE YAANDIKWE KWA KUZINGATIA YAFUATAYO:**
Tarehe ya mwisho kuwasilisha maombi ni siku ya **jumatatu 12, January , 2026 saa 4:00 asubuhi (Saa nne kamili asubuhi)** Maombi ya Kotesheni yawasilishwe Ofisi ya Chama kikuu **[SHIRECU (1984) LTD]** yafungwe ndani ya bahasha kwa **LAKIRI** .

Barua iandikwe kwa;

**MENEJA MKUU,**
**SHIRECU (1984) LTD,**
**S. L. P. 349,**
**SHINYANGA.**

**Kwa maelekezo zaidi kuhusiana na Zabuni hii tafadhali usisite kuwasiliana nasi kwa kupitia simu namba 0654 17 4669 au barua pepe info@shireculimited.co.tz**

**TANGAZO HILI LIMETOLEWA NA**

N.M
..........................................
**Naomi Mayega Chaba**

**MWENYEKITI WA UONGOZI WA BODI**

**SHINYANGA CO – OPERATIVE UNION (1984) LTD**

SHINYANGA REGION CO-OPERATIVE UNION (1984) LTD. P. O. BOX 349